

TAKUKURU TEMEKE YAKAMATA WATATU KWA RUSHWA, YAWAFIKISHA MAHAKAMANI

Na Tezra Nkonya, Dar es Salaam

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Temeke imewafikisha watu wanne kwenye Mahakama ya Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam Februari 2, 2018 kwa makosa mawili ya kuomba na kupokea rushwa.

Akiongea na waandishi wa habari kabla ya kuwafikisha mahakamani, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Temeke, Pilly Mwakasege aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Emmanuel Stephen Kobelo ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Jangwani; Ally Matola Ally ambaye ni mfanyabishara wa shughuli za bima kampuni ya Equalmalk Ltd; Julius Fredrick Chilumba ambaye ni Afisa Magereza mstaafu akifahamika pia kwa jina la Joseph Philip Chiluba na Dorothy John Magige

Mwakasege alisema Kobelo, Ally na Chilumba walikamatwa na maafisa wa TAKUKURU katika mtego wa rushwa Januari 30, 2018 saa 2:30 usiku maeneo ya Jet Lumo, jijini Dar es Salaam baada ya kupokea rushwa ya shilingi milioni mbili kati ya shilingi tatu walizoshawishi awali kutoka kwa mfanyabiashara mmoja wa madini ili wasimchukulie hatua kwa kile walichodai kuwa kosa la kushirikiana na wageni kutoka nje ya nchi kufanya biashara haramu ya madini ya dhahabu na almasi.

Washtakiwa walifikishwa mahakamani mbele ya Kaimu Hakim Mfawidhi wa Mahakama ya wilaya ya Temeke, Suzan Kihawa na kusomewa shitaka moja la kushawishi rushwa ya shilingi milioni tatu na moja la kupokea rushwa ya shilingi milioni mbili.

Upande wa mashtaka ulioongozwa na waendesha mashtaka wa TAKUKURU Mwanakombo Rajab, Thuwaiba Husein na Mbumi **Kisiki** uliarifu Mahakama kuwa washtakiwa walishawishi rushwa ya shilingi milioni tatu kutoka kwa mlalamikaji Januari 26, 2018 na kupokea rushwa shilingi milioni mbili kutoka kwa mlalamikaji Januari 30, 2018 ili wasimchukulie hatua kwa kile walichodai kuwa kosa la kushirikiana na wageni kutoka nje ya nchi kufanya biashara haramu ya madini ya dhahabu na almasi.

Upande wa mashtaka uliambia mahakama kuwa washtakiwa walitenda makosa ya kuomba na kupokea rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

Washtakiwa walikana mashtaka dhidi yao na walipelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ya kuwa na wadhamini wawili wanaoaminika, mmoja akiwa mtumishi wa **Serikali**. Kesi imeahirishwa hadi Februari 15, 2018 itakapokuja kwa kutajwa kwa kuwa uchunguzi haujakamilika.

Awali akiongea na waandishi wa habari, Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Temeke aliwatahadharisha watumishi wa umma na wananchi wote kwa ujumla kutojihusisha na vitendo vya rushwa na atakayefanya hivyo atachukuliwa hatua za kisheria. Mwakasege pia aliwaasa wananchi wote kuichukia rushwa na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kufika ofisi za TAKUKURU au kwa kutumia bure huduma ya simu ya dharura namba 113 inayopatikana ama kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwenda 113 au kupiga *113#.



Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Temeke, Bi. Pilly Mwakasege akiongea na waandishi wa habari Februari 2, 2018.